

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**



Dar es Salaam
24 Aprili, 2026

C Barua pepe: press@ikulu.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

**RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN APOKEA HATI ZA UTAMBULISHO
KUTOKA KWA MABALOZI WANANE, AWEKA MSISITIZO KWENYE
DIPLOMASIA YA KIUCHUMI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amepokea Hati za Utambulisho kutoka kwa Mabalozi wanane wanaowakilisha nchi zao hapa nchini, katika hafla iliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam.

Mabalozi waliowasilisha hati zao ni Mhe. Salam Abu Sharar wa Palestina, Mhe. Catherine Karemu wa Jamhuri ya Kenya, Mhe. Jovica Tupalovic wa Jamhuri ya Serbia, Mhe. Maes Ennio wa Jamhuri ya Côte d'Ivoire, Mhe. Luteni Jenerali Mstaafu Peter Kakowou wa Jamhuri ya Sierra Leone, Mhe. Gideon Behar wa Israel, Mhe. Dzmitry Krasouski wa Jamhuri ya Belarus na Mhe. Paul Evans Aidoo wa Jamhuri ya Ghana.

Katika mazungumzo yake na mabalozi hao, Rais Dkt. Samia alieleza dhamira ya Tanzania kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika nyanja za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kibiashara, huku akisisitiza umuhimu wa nchi za Afrika kuongeza thamani ya rasilimali zake kupitia uzalishaji wa pamoja.

Aidha, Rais Dkt. Samia alitaja maeneo ya kipaumbele ya ushirikiano kuwa ni pamoja na maendeleo ya miundombinu ya maji na umwagiliaji, pamoja na kukuza viwanda kwa lengo la kuongeza tija na ajira.

Mheshimiwa Rais aliwahakikishia mabalozi hao kuwa Tanzania itaendelea kuwa mshirika wa kuaminika, akisisitiza kuwa milango iko wazi kwa ushirikiano wa karibu zaidi unaolenga kukuza uchumi wa pande zote kupitia diplomasia ya kiuchumi.

Kwa upande wao, mabalozi walimpongeza Rais Dkt. Samia kwa uongozi wake thabiti na juhudi zinazoendelea katika kuimarisha mazingira ya uwekezaji, amani na utulivu nchini.



Vilevile, walionesha utayari wa nchi zao kuendeleza ushirikiano na Tanzania katika maeneo ya kimkakati.

Mazungumzo hayo pia yaligusia masuala ya diplomasia ya kikanda na usalama wa dunia, yakisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kukabiliana na changamoto za pamoja.

MAELEZO KWA MHARIRI

Uwasilishaji wa Hati za Utambulisho ni utaratibu rasmi wa kidiplomasia unaomruhusu balozi kuanza rasmi majukumu yake katika nchi mwenyeji.

Tanzania imeendelea kuimarisha diplomasia ya kiuchumi kama nyenzo ya kuvutia uwekezaji, kukuza biashara na kuharakisha maendeleo ya viwanda.



Bakari S. Machumu

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu